# OFISI YA RAIS
# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
# SHULE YA SEKONDARI MABIRA

**MAELEKEEZO YA KUJIUNGA NA MASOMO YA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021**
**(JOINING INSTRUCTIONS)**

**Simu No. 0763 068 014 au 0625 467 971 (Mkuu wa shule)**
**au 0688405013 au 0755313666 au 0621 836 149 (Makamu Mkuu wa shule)**
**au 0766 286 070 au 0622 573 213 (Mwalimu wa nidhamu na malezi)**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**SHULE YA SEKONDARI MABIRA**

**S. L. P 245**
**KYERWA**
**TAREHE 19/12/2020**

Kumb. Na.KGR/HW/KYR/MSS/J.I/28

Ndugu Mwanafunzi…......................
S/MSINGI…...................................

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MABIRA ILIYOPO WILAYA YA KYERWA MKOA WA KAGERA MWAKA 2021**

**1.0 Utangulizi**

Natumia fursa hii kukujulisha na kukupongeza kuchaguliwa kujiunga na Shule ya Sekondari Mabira kidato cha kwanza mwaka 2021 Ninakukaribisha sana nikitumaini kuwa nafasi hii ya pekee utaipokea na kuitumia kwa manufaa yako mwenyewe, wazazi na Taifa kwa ujumla **KARIBU SANA**

Shule ya Sekondari Mabira iliyopo katika Mkoa wa Kagera, Wilaya ya Kyerwa, ipo upande wa kaskazini umbali wa km 30 kutoka mji mdogo wa Nkwenda, upande wa mashariki km 60 kutoka mji mdogo wa Kaisho, upande wa magharibi km 54 kutoka mji wa Kayanga kwa kupitia barabara ya Rwambaizi. Usafiri unaopatikana kutoka maeneo tajwa hapo juu ni wa magari madogo ya abiria.

Muhula wa kwanza, masomo yataanza tarehe 11/01/2021 Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 18/01/2021

**2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**2.1 SARE YA SHULE**

Sare ya shule hii ni kama ifuatavyo:

**(a) Wavulana**

(i) Suruali 2 nyeusi zenye heshima, mfuko mmoja wa nyuma na miwili pembeni. (Tutazikagua kabla ya kumpokea)
(ii) Shati mbili nyeupe aina ya tetron mikono mifupi
(iii) Viatu vyeusi (Ngozi ) jozi moja vinavyofungwa kwa kamba za viatu, vyenye kisigino kifupi
(iv) Soksi nyeusi jozi mbili.
(v) Mkanda wa suruali usiopungua na usiozidi inchi moja na nusu.
(vi) Sweta ya shule yenye rangi ya njano na nembo ya shule. (Angalia za wanafunzi wa kidato cha pili na kuendelea)

(vii) T-shirt yenye maandishi ya **" SHULE YA SEKONDARI MABIRA, KUSONGA MBELE KUVUKA WOTE"** mgongoni. Maandishi yaandikwe kama ifuatavyo: neno **SHULE YA SEKONDARI MABIRA** liwe katika mviringo na **KUSONGA MBELE KUVUKA WOTE** yawe chini ya mviringo huo. Unashauriwa kutazamia T-shirt za wanafunzi wa madarasa ya kidato cha pili hadi cha nne. T-shirt iwe na nembo ya shule Kifuani upande wa kushoto. (ANGALIA PICHA UKURASA WA KWANZA WA FOMU HII)

(**b) Wasichana**

(i) Shati mbili aina ya tetron mikono mifupi
(ii) Sketi mbili nyeusi, ndefu hadi chini ya magoti mpaka kwenye soksi, ziwe pana (zisibane mwili).Tutazikagua kabla ya kumpokea. Ziwe na malinda madogo yenye upana wa inchi mbili.

(iii) Viatu vyeusi vya Ngozi jozi moja vinavyofungwa kwa kamba za viatu.
(iv) Soksi ndefu (Stocking) jozi 2 nyeupe zinazoweza kufika usawa wa magoti
(v)Sweta ya shule yenye rangi ya njano na nembo ya shule (Angalia za wanafunzi wa kidato cha pili na kuendelea)
(vi) Jalabib rangi nyeupe inayofanana na shati kwa (wanafunzi wa kiisalamu)
(vii) T-shirt yenye maandishi ya **" SHULE YA SEKONDARI MABIRA, KUSONGA MBELE KUVUKA WOTE"** mgongoni. Maandishi yaandikwe kama ifuatavyo: neno **SHULE YA SEKONDARI MABIRA** liwe katika mvuringo na **KUSONGA MBELE KUVUKA WOTE** yawe chini ya mvuringo huo. Unashauriwa kutazamia T-shirt za wanafunzi wa madarasa ya kidato cha pili hadi cha nne. T-shirt iwe na nembo ya shule Kifuani upande wa kushoto. (*ANGALIA PICHA UKURASA WA KWANZA WA FOMU HII*)

(c) **SARE YA MICHEZO**

**(a) Wavulana**

(i) Bukta moja rangi nyekundu.
(ii) T-shirt moja rangi ya njano.
(iii) Viatu aina ya raba jozi moja.
(iv) Soksi ndefu za michezo.

**(b) Wasichana**

(i) Sketi moja rangi ya bluu na bukta moja rangi ya bluu.
(ii) T-shirt moja rangi ya njano.
(iii)Viatu aina ya raba jozi moja.
(iv) Soksi ndefu za michezo.

**2.2 VIFAA VYA DARASANI**

i. Daftri kubwa 10 (counter book 2 quire au kubwa zaidi)
ii. Kalamu za wino 5
iii. Penseli 3
iv. Mkebe 1 wa hesabu (Set)
v. Rula 1
vi. Daftari ndogo 10 za kufanyia mazoezi ya darasani.

2.3 Kwa suala la matibabu, shule inatoa huduma ya kwanza tu na mwanafunzi akihitaji matibabu zaidi mzazi wa mwanafunzi husika atagharimia matibabu yake.

2.4 Mzazi atagharimia nauli ya kwenda shuleni na kurudi nyumbani wakati wa likizo. Pia atamnunulia mahitaji binafsi kama vile godoro, mashuka, beseni na vifaa vingine vya matumizi binafsi ya mwanafunzi. Vifaa muhimu kwa wanafunzi ni pamoja na:

1. Gauni mbili ndefu za solo rangi ya kijani zisizobana mwili (***Kwa wasichana tu***).
2. Suruali mbili rangi ya damu ya mzee na T.shirt mbili zenye kola rangi ya zambarau kwa ajili ya kuzivaa baada ya muda wa darasani (***Kwa wavulana tu***).
3. Shuka pair 2 rangi ya blue au pink na taulo.
4. Godoro dogo futi 2 na nusu au futi 3, mto na blanket.
5. Sanduku la mbao, tochi na betri.
6. Sahani na bakuli za bati, kijiko na kikombe.
7. Ndala (kandambili) au yebo.
8. Mafuta ya kujipaka, brush ya viatu, dawa ya viatu, dawa ya meno na mswaki.
9. Ndoo ndogo, beseni na dumu la lita 5.
10. Peds kwa ajili ya wasichana ambao umri wao ni mkubwa (waliopevuka)

***NB: Mwanafunzi yeyote hataruhusiwa kuwa na nguo nyingine tofauti na sare za shule zilizoelekezwa hapo juu.***

**2.5 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.**

Shule inaendeshwa kwa mjibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya elimu, Sayansi, teknolojia na

ufundi yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya Rais tawala za mikoa na serikali za mitaa yenye jukumu la usimamizi na uendehaji wa elimu. Unatakiwa kuzingatia sheria za shule kama zilivyoelezwa hapa chini:

**SHERIA ZA JUMLA**

1. Kila mwanafunzi anatakiwa kutii sheria za shule, kuheshimu walimu, wafanyakazi wasio walimu,wageni na wazazi wanaoitembelea shule,viongozi wa wanafunzi na wanafunzi wengine wote. Ni lazima kila wakati kufuata taratibu zinazowekwa na vilevile kuwa na tabia nzuri
2. Kila mwanafunzi ni lazima kuvaa sare ya shule (school uniform) akiwa shuleni na anapokuwa na ruhusa rasmi ya kutoka nje ya shule.
3. Ni muhimu na ni wajibu wa kila mwanafunzi kuhudhuria na **KUWAHI** bila kuchelewa kwenye masomo, kipindi cha kazi, na shughuli yoyote ya shule kila wakati (punctuality). Unatakiwa kuwa umefika shuleni saa 1.00 asubuhi na kuondoka saa 10. 00 alasiri kutegemeana na maelekezo ya mwalimu wa zamu. Kila wakati zingatia ratiba ya shule.
4. Kila mwanafunzi wa shule hii, hana budi kuomba ruhusa maalumu anapotaka kwenda nje ya shule kama nyumbani kwao au penginepo. Ruhusa ya kwenda nje ya shule au hospitali inatolewa na mkuu wa shule au makamu wake.
5. Kila mwanafunzi anatakiwa kujiheshimu yeye binafsi na kuwaheshimu watu wengine wote kama anavyopenda aheshimike
6. Ni wajibu wa kila mwanafunzi kutunza na kulinda SIHA na usafi wake binafsi na mazingira yote (ndani na nje ya shule yake hasa madarasani, vyoo na viwanja vya shule ) . Takataka zisitupwe ovyo.
7. Ugonvi, hila na matusi yoyote ya kusema au kuandika hayatakiwi kabisa.
8. Kila mwanafunzi ni lazima aheshimu na kutunza mali yoyote ya shule, mali yake binafsi na mali ya wenzake . Ni kosa kubwa kuharibu mali ya shule au ya mtu mwingine yeyote.
9. Wizi wa aina yoyote ile ni kosa kubwa mno. Mwizi na mdokozi hataruhusiwa kuendelea na masomo.
10. Kila mwanafunzi ni lazima aepuke na achukie vitendo vya aina yoyote ya **UONGO, UASHERATI, ULEVI, UVUTAJI SIGARA, UTUMIAJI MADAWA YA KULEVYA NA UTORO.**
11. Kila mwanafunzi lazima aheshimu kazi za mikono kama vile anavyoheshimu masomo yake . Uzembe ,jeuri, na ubishi wenye lengo la kukwepa kutimiza wajibu hauruhusiwi kabisa .
12. Bangili, mikufu, vibandiko, kofia pamoja na (Jugle hats), kanda mbili, mikanda mipana na mingineyo yenye rangi tofauti na nyeusi hairuhusiwi kamwe kuvaliwa na wanafunzi wakiwa katika vazi la shule ***isipokuwa kwa kibali maalumu kutegemeana na hali ya mwanafunzi husika***.
13. Makosa yafuatayo yatakufanya usimamishwe ama kutolewa kabisa shuleni wakati wowote;
    - Wizi
    - Ulevi wa pombe
    - Uvutaji wa sigara na utumiaji wa madawa ya kulevya kama vile bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika
    - Makosa ya jinai
    - Uharibifu wa makusudi wa mali ya umma
    - Kupiga au Kupigana (Ugonvi)
    - Kuoa au kuolewa bado mwanafunzi
    - Ubakaji
    - Uasherati (matendo ya ngono) na ushoga aidha kwa kushiriki au kuwa wakala (Agenti)
    - Utoro
    - Kudharau bendera ya taifa
    - Kukataa adhabu kwa makusudi
    - Kuwa na simu ya mkononi au ya aina yoyote ile.
    - Kushawishi/kushiriki katika migomo au kwa namna yeyote nyingine kushiriki kuvunja amani na usalama wa shule na watu
    - Kupata mimba, kutoa mimba kushiriki kutoa mimba au kumpa mimba mwanafunzi au raia
14. Huruhusiwi kutumia lugha tofauti na ya kingereza (na Kiswahili katika somo la Kiswahili tu)
15. Mwanafunzi akiwa na shida/tatizo ajulishwe mwalimu wa darasa, mwalimu wa zamu, au mwalimu mlezi na sehemu nyingine inayohusika (mfano: mwalimu wa taaluma, makamu mkuu wa shule au mkuu wa shule).
16. Mwanaafunzi haruhusiwi kuja shuleni na simu, radio, kamera na vifaa vingine vya jamii hiyo

**SHERIA ZA MADARASANI**

1. Kila mwanafunzi anapaswa kukaa darasani katika nafasi yake aliyopangiwa
2. Mwanafunzi hataruhusiwa kukaa darasani wakati wa masomo kama hana sare ya shule
3. Kelele za aina yoyote haziruhusiwi
4. Wanafunzi lazima wasimame mwalimu au mgeni wa shule aingiapo darasani au kutoka.
5. Wanafunzi hawaruhusiwi kukalia viti vya walimu
6. Darasa litafaguliwa kila siku asubuhi kwa kufuata utaratibu wa ufagiaji utakaopangwa.
7. Mwanafunzi itambidi afuate mahudhurio ipasavyo. Kukosa mahudhurio ya vipindi bila ruhusa ni kosa na linastahili adhabu. Endapo mwanafunzi hatahudhuria masomo kwa kipindi cha siku zaidi ya 90 atakuwa amejifukuza shule
8. Mwanafunzi atakaa darasani muda wote anaopaswa kukaa darasani. Kuzulura nje wakati wengine wapo darasani ni kosa.

NB: Msisitizo mkubwa na vipaumbele vya Mabira Sekondari ni "**TAALUMA SAFI, NIDHAMU SAFI, MICHEZO SAFI"** ndani ya **MAZINGIRA SAFI**. Hivyo unatakiwa kuwa makini kufuata taratibu, kanuni na sheria za shule zilizotajwa ikiwa ni pamoja na maagizo mengine utakayopewa kwa ajili ya kuongeza ***TIJA*** ya malezi

**ADHABU**

1. Walimu na viranja wa shule waweza kumuadhibu mwanafunzi anayevunja sheria na kanuni za shule au taratibu zinazotolewa mara kwa mara
2. Adhabu zitatolewa kulingana na kosa na uwezo wa kuteleleza
3. Kwa makosa makubwa adhabu itatolewa na bodi ya shule / mkuu wa shule

**3.0 MAMBO MENGINE MUHIMU**

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maelekezo haya na kuyatekeleza kikamilifu. Wakati wa kuripoti shuleni, rudisha fomu hii ikiwa imejazwa vizuri katika viambatanisho A, B na C.

**KARIBU SANA**

…………………………………..

**DANFORD A. NUVYE**

**MKUU WA SHULE**

**SHULE YA SEKONDARI MABIRA**
**KIAMBATANISHO " A"**

**FOMU YA KUKUBALI NA KUTII SHERIA ZA SHULE**

ANWANI……………………………………………………

………………………………………………………………

………………………………………………………………

…………………………………………………………………

Mimi…………………………………………………………………(Jina la mwanafunzi) nimepokea barua ya kuingia kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Mabira kuanzia tarehe 07/01/2021hadi 18/01/2021Nakubali nafasi hiyo kwa moyo mkunjufu. Baada ya kusoma na kuelewa sheria za shule, naahidi kuwa nitatii sheria hizo kama zilivyoainishwa katika fomu ya maagizo ya kujiunga na shule ya sekondari Mabira. Endapo nitashindwa kutii sheria hizo hatua inayostahili ichukuliwe dhidi yangu

Natoa ahadi hii mbele ya Mzazi /mlezi wangu ambaye ametia sahihi yake hapa chini.

Jina la mwanafunzi ………………………………………sahihi……………………

Mimi………………………………(Jina la mzazi /mlezi) ambaye ni mzazi /mlezi wa mwanafunzi aliyetajwa hapo juu, nakubali mwanangu ajiunge kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Mabira na kutii sheria za shule na naahidi kushirikiana na shule ili kuhakikisha tunatoa malezi bora kulingana na sheria hizo na nyingine ambazo hazikutajwa pia.

Iwapo sitakuwepo mimi likitokea tatizo ninaweza kuwakilishwa na

1. ……………………………………….ambaye ni ………………………………..

2. ……………………………………..……. ambaye ni ………………………………..

(Eleza uhusiano wako na wawakilishi hao)

Jina la mzazi / mlezi …………………………………

Sahihi ………………………………………………

Tarehe……………………………………………

**SHULE YA SEKONDRI MABIRA**

**KIAMBATANISHO B**

**MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI**

1. JINA KAMILI ……………………………………………………………………(Kama ilivyo kwenye TSM 9)
2. Tarehe ya kuzaliwa ……………………………………………………………
3. Mahali alipozaliwa : Wilaya………………………………………………………………
4. Kijiji ………………….kata……………(mwanafunzi alete shuleni nakala ya cheti cha kuzaliwa)
5. Anwani ya nyumbani ni …………………………………………………………..

6. Dini yake……………………………………………………………
7. Mahali unapoishi ni umbali gani kutoka shuleni ? KM …………………………………
8. **WAZAZI**: Jina na anwani ya baba ………………………………………………….
   Anaishi /Amefariki (kata isiyohusika). Ni raia wa nchi ipi? Itaje.............................(Tanzania/nchi nyingine)

Jina na anwani ya mama ………………………………………………

Anaishi / Amekufa(kata isiyohusika). Ni raia wa nchi ipi? Itaje.............................(Tanzania/nchi nyingine)

Jina na anwani ya MLEZI…………………………………………………………
(Kama siyo baba na mama) Ni raia wa nchi ipi? Itaje.............................(Tanzania/nchi nyingine)

9. **<u>MAELEZO YA AFYA</u>**

Eleza kama una tatizo lolote linalohitaji msaada au linaloweza kuathiri utendaji wako wa kazi za kila siku pamoja na maendeleo yako ya masomo. Maombi maalumu yadhibitishwe na daktari

…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………

10. Uongozi wa kijiji (kwa udhibitisho)

Jina la mwenyekiti wa kijiji ………………………………

Anwani yake …………………………………………………Tarehe…………….

11 Uongozi wa kata (kwa uthibitisho)

Jina la Afisa mtendaji wa kata……………………………………

Kata……………………………………

Sahihi…………………………………

Muhuri……………………………

**KIAMBATANISHO C**

**SHULE YA SEKONDARI MABIRA**

**HATI YA UTHIBITISHO WA TABIBU (anayetambuliwa na serikali)**

Nathibitisha kwamba nimemchunguza mwanafunzi

Jina……………………………………………………………………………………………………
…………………

Kinyesi……………………………………….Matokeo……………………………

Mkojo………………………………………… Matokeo……………………………

Macho……………………………………… Matokeo……………………………

Damu………………………………………Matokeo…………………………..

Mapigo ya moyo…………………………...Matokeo……………………………

Urine Pregnancy Test (UPT)………………………Matokeo ……………………………..

**MATIBABU** Yafuatayo yametolewa (kama ni ugonjwa wa kudumu eleza)
………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………
……………………………………
………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………
…………

Jina la tabibu……………………………………

Sahihi………………………………………….…

Tarehe…………………………………………..

Muhuri ……………………………………